

**Swahili transcript:**

Na, sherehe hii ni nzuri sana kwa sababu inamsaidia sana binti katika kuanza majukumu halisi ya kifamilia na mara nyingi aah! Kama nilivyosema niwakina mama ndio ambao wanaandaa, kwa hiyo siku hiyo ya kitchen party aah! wanaume wanakuwa hawapo, hata wazazi kama wa binti labda baba na kaka zake na ndugu na nani, wajomba labda wote wanakuwa hawaruhusiwi katika sherehe hiyo ya kitchen party. Kwa hiyo siku hiyo ya kitchen party mara nyingi aah! Tunavaa khanga, khanga nii, ni vazi rasmi la kitanzania, tunavaa khanga katika kitchen party, wengine huwa wanashona ile khanga, wengine huwa wana wanaji tunasema wanajitandia, wanachukua ile khanga wanajirushia begani, au wengine pia wanafunga ile khanga, na nyingine labda wanajifunika, inategemea na, aah! Na jinsi mtu anavyoamua kufanya. Na mara nyingi wale bibi aah! bibi harusi mtarajiwa ambaye ndiye binti anayefanyiwa hiyo kitchen party huwa mara nyingi huwa anashona ile khanga, wengine wanamfunga katika mtindo mzuri ambao anatoka anapendeza vizuri sana na anakuwa pamoja na, mmh! Kwa neno la kiingereza tunasema matron, anakuwa pamoja na matron wake, kwa hiyo sherehe inaanza hapo, wanaandaa vyakula mbalimbali, kwa mfano vyakula mbalimbali vya kitanzania, aah! Vinyaji mbalimbali, pamoja na muziki na inategemea kama ni wakristo mara nyingi wanaandaa miziki ya kikristo, au tunasema labda nyimbo za injili. Kwa hiyo mara nyingi inakuwa hivyo, kwa hiyo wakati ule mara nyingi inafanyika muda wa jioni, labda kuanzia saa tisa mchana, aah! saa tisa alasiri na kuendelea, labda wengine mpaka labda saa mbili za usiku wanafanya hii sherehe ya kitchen party. Kwa hiyo sherehe inavyokuwa ni kwamba aah! wakina mama wanakuwa wamekusanyika mahali, na mara nyingi siku hizi huwa inafanyika katika kumbi, kumbi za sherehe, kwa hiyo ule ukumbi unapambwa vizuri kutokana na zile rangi ambazo bibi harusi anavaa au zile rangi ambazo khanga za wale wakina mama wanavaa siku hiyo pamoja na mapambo mengine tu mazuri, kwa hiyo ukumbi unapambwa vizuri na inaandaliwa sehemu maarufu kwa ajili ya kukaa yule bibi harusi pamoja na tunaita mpambe, mpambe wake, ambaye kwa kiingereza tunasema matron, lakini mara nyingi tumezoea kusema mpambe, kwa hiyo bibi harusi anakaa pale

na mpambe wake, na wakina mama wanakaa upande mwingine, wakina mama pamoja na mabinti ambao ni rika la yule binti ambaye anafanyiwa kitchen party. Mara nyingi watoto wadogo hawaruhusiwi pia katika sherehe hizi za kitchen party. Kwa hiyo kunakuwa na nasaha mbalimbali ambazo wakina mama ambao wameolewa wanazitoa kwa yule binti, kwa sababu,kiutamaduni Tanzania, ni kwamba mama anategemewa ndiye kuwa mwalimu wa kwanza wa familia, kwamba mama yeye ndiye anayewalea watoto, anayewatunza watoto,anayefanya shughuli za pale nyumbani,shughuli za usafi na katika kupika, kui pikia familia yake,ni mama ndiye ambaye anafanya kazi hizo. Ni tofauti kidogo na mfano huku Marekani na sehemu nyingine za Ulaya,utakuta baba pia nae anapika, au baba anasafisha mtoto,lakini katika,kiutamaduni wa kitanzania ni mama ndiye ambaye analea familia, ni mama ambaye ndiye anategemewa kuwa yeye ndiye ambaye anapika kwa ajili ya watoto,anafanya usafi, anasafisha nyumba, anaweka kila kitu safi, katika hali ya usafi na kuitunza familia, ni mama ndiye ambaye jukumu kubwa la kuitunza familia katika utamaduni aah!wa kitanzania.

**English translation:**

As I said earlier, this celebration is to help a young lady who is getting ready to get married, and it is good because it helps her get some important kitchen items. Men are not allowed to attend; not even her father, brothers, uncles, cousins and other relatives. It is only women who prepare and attend this celebration. During the day of the kitchen party, we wear *kanga*. *Kanga* is the official cloth of Tanzania. We wear *kanga* when we celebrate a kitchen party. Some have dresses made from *kanga* cloth; others just wrap it and others put it on their shoulder. It depends on how they want to wear *kanga*. The bride-to-be usually makes a dress, or women will wrap her in a very unique way and she looks very pretty. She is always accompanied by her matron, and so the celebration starts. They make good, delicious food, drinks and music that depends on the faith of the bride-to-be. If she is a Christian, they will have what we call gospel music. A kitchen party is always held in the late afternoon, for example from 3:00 p.m. to 8:00 p.m. So women gather in the hall which they decorate with colors and other decorations which resemble the colors of the *kanga* they are wearing. They make a nice place for the bride to sit with

her matron. They also prepare a place where other women and young ladies who are age mates of the bride will sit. Children are not allowed to attend a kitchen party. After that, women who are married give advice to the bride-to-be because, traditionally in Tanzania, the mother is considered to be the first teacher of her family. She is the one to take care of her children, to cook for her family, and to clean. It is different from here in America and other places in Europe where you find a father who cooks and washes his child. But in Tanzania, it is traditional that the mother is the one to take care of her children, to cook for them, to clean and keep things in order at home. She is expected to be efficient in her home. That is why they give her kitchen tools to enable her to cook for her family. They also give her cleaning items to help her be on top of things. That is the main purpose of a kitchen party.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated